# HALMASHAURI YA WILAYA YA MUHEZA

**SHULE YA SEKONDARIMLINGANO**
S.L.P 281 MUHEZA
TAR …………………
NAMBA ZA SIMU: 0782 411 476
: 0652 363610

**MWANAFUNZI** ………………………………………………
S.L.P ………………………

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MLINGANO WILAYA YA MUHEZA**

1.0. Nina furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza katika shule ya sekondari Mlingano ambayo iko km.12 toka stendi ya Muheza. Usafiri wa basi kutoka mjini Muheza unapatikana katika kituo cha mabasi cha Muheza. Nauli ni shilingi **1000/=** mpaka Mkanyageni. Kutoka Mkanyageni mpaka shuleni ni umbali wa kilometa 1½ usafiri wa pikipiki (boda boda) upo na nauli ni shilingi elfu moja **(1,000/=).** Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **07/01/2024** kwa wanafunzi wa bweni. Na **08/01/2024** kwa wanafunzi wa kutwa.

**2.0. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.0.1. SARE ZA SHULE**

**WAVULANA**

**a)** Shati jeupe la mikono mifupi liwe na alama ya moja Nyeusi begani kuonesha ni kidato cha kwanza
**b)** Viatu vya ngozi vyeusi visigino vifupi, vya kamba (jozi mbili).
**c)** Soksi rangi nyeusi jozi mbili na zaidi
**d)** Raba za michezo
**e)** Bukta za michezo rangi yoyote isiyokuwa na maandishi.
**f)** Mkanda mweusi wa ngozi rangi nyeusi
**g)** Sweta la rangi nyeusi lenye shingo ya V mbele

**WASICHANA**

a) Sketi zaidi ya moja, rangi ya damu ya mzee ndefu usawa wa kisigino na iwe ya rinda box mbele na nyuma
b) Shati rangi nyeupe zaidi ya moja, liwe mikono mifupi liwe na alama ya moja ya damu ya mzee kuonesha ni kidato cha kwanza
c) Viatu vyeusi jozi mbili vyenye kamba na visigino vifupi/simple nyeusi zisizo na urembo
d) Soksi rangi nyeupe jozi zaidi ya mbili
e) Rangi ya hijab ni kitambaa cheupe kinachofanana na shati la shule iwe ndefu
f) Nusu kanzu kwa wanaovaa hijabu ni rangi nyeupe iwe ndefu
g) Fulana rangi ya njano isiyo na maandishi kwa ajili ya michezo
h) Sweta la damu ya mzee yenye shingo ya V mbele

i) Kwa wanafunzi wenye ulemavu wa ngozi (albino) waje na mafuta yao na kofia za jua na mashati yao yawe ya mikono mirefu
j) Chandarua cheupe
k) Raba za michezo
l) Aje na nakala ya cheti cha kuzaliwa na NIDA mzazi au mlezi

**WASICHANA (BWENI)**

1. Godoro ft 3. Upana inchi 3 hadi 4
2. Godoro linalohitajika liwe ni Comfy au godoro la Dodoma
3. Shuka mbili rangi ya **pink**, mto, foronya rangi ya **pink** na chandarua cha mbu cheupe.
4. Mahitaji kwa ajili ya usafi binafsi
5. Fedha za matumizi
6. Sahani, bakuli, kijiko, kikombe na chupa ya maji ya kunywa iliyo tupu na safi au yenye maji safi na salama yenye ujazo wa lita 1kwa ajili ya kuhifadhia maji ya kunywa.
7. Taulo na kanga na(taulo za kike )
8. Sanduku la bati zito (trunk) na begi la safari
9. Gauni la kushindia rangi ya zambarau kitambaa cha satini, gauni la solo refu. Idadi yoyote ni lazima.
10. Ndoo ya kuogea na maji ya kunywa (ndoo mbili ndogo na kubwa moja)
11. Track suit rangi ya dark blue ni lazima (Jozi mbili)
12. Net **nyeupe** ya mbu
13. Aje na bima ya afya ni lazima
14. Raba za michezo
15. Sare zote za wanafunzi ziwekwe alama ya utambuzi. Kwa mfano jina lake

**NB: Nguo za nyumbani haziruhusiwi kuingia bwenini.**

**2.0.2. SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII**

Shule imeanzishwa kwa mujibu wa sheria Na.25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo mara baada ya kuripoti shuleni;

a) Heshima kwa viongozi, wazazi wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
b) Mahudhurio mazuri katika shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu.
c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni (Preparation).
d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyinginezo utakazopewa.
e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule.
g) Kuvaa sare ya shule wakati wote.
h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
i) Mzazi atagharamia matibabu iwapo mwanae ataumwa, shule haina zahanati. **Hivyo mzazi unaombwa kumkatia mtoto bima ya afya**
j) Atakaye husika kuhusu ufuatiliaji wa maendeleo ya wanafunzi ni yule aliyeandikwa kwenye fomu ya historia ya mwanafunzi.
k) Shule haina chakula maalumu kwa wagonjwa (***special diet*****).**

l) Hairuhusiwi mwanafunzi kubadilisha dini awapo hapa shuleni labda kwa kibali cha maandishi kutoka kwa mzazi aliyeandikishwa shuleni.

**m) Hakuna kutembelewa kwa wanafunzi wa bweni (visiting day)**

**2.0.3. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA UFUKUZWE SHULE**

1. Wizi
2. Uasherati na ushoga
3. Ubakaji
4. Ulevi na matumizi ya madawa ya kule vya kama vile uvutaji wa bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k.
5. Kupigana au kupiga
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
7. Kudharau Bendera ya Taifa
8. Kuoa au kuolewa
9. Kumpa mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.
10. Kutoa mimba
11. Kugoma, kuchochea ama kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu.
12. Kukataa adhabu kwa makusudi.
13. **Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi**

**2.0.4 ZANA ZA KAZI**

1. Daftari zaidi ya 22 (book 12.203x254)
2. Kalamu za wino, risasi na rula
3. Mkebe wa vifaa vya hesabu (mathematical set) na dictionary
4. Begi la madaftari ni lazima kila mwanafunzi awe nalo

**3.0.2. VIFAA VYA USAFI**

5. Wanafunzi wa bweni ndoo 1 kubwa, kwanja 1, fagio moja refu na jembe lenye mpini.
6. Wanafunzi wa kutwa ndoo 1 kubwa, fagio moja la chelewa refu,kwanja na jembe lenye mpini.

**3.0. TARATIBU ZA KUKAMILISHA KABLA YA KUJA SHULENI**

Ni muhimu uje na fomu ambazo zimeamabatanishwa zikiwa zimekamilika.

1. Fomu ya historia ya mwanafunzi
2. Fomu ya kukubali nafasi ya mwanafunzi
3. Fomu ya kiapo cha uraia
4. Fomu ya maelezo ya daktari. Vyote hivyo vitakaguliwa kabla ya kuandikishwa.

**MENGINEYO**

1. Sheria za shule zimeambatanishwa.
2. Haturuhusu kubadili jina.
3. Lugha ya mawasiliano darasani na nje ni kingereza.

**MWISHO.**

Kwa niaba ya Wizara, Shule na mimi mwenyewe, ninakukaribisha Shule ya Sekondari Mlingano.

Ni matumaini yangu kuwa utaitumia vyema nafasi hii.

______________________

**MNZAVA.N.M**
**MKUU WA SHULE**

O/R TAMISEMI

SHULE YA SEKONDARI MLINGANO

HISTORIA YA MWANAFUNZI

(***Ijazwe kwa herufi kubwa kwa kutumia muandiko wako***)

1. Jina la Mwanafunzi …………………………………
2. Tarehe ya kuzaliwa ………………………Wilaya…………………
3. Kabila …………………Dini/Dhehebu ………………………
4. Jina la Baba ………………………Hai/Amefariki…………………
5. Jina la Mama ………………………Hai/Amefariki …………………
6. Jina la Mzazi /Mlezi atakaye gharamia mahitaji yako shuleni ……………anuani yake ……………Namba ya simu ………………
7. Uhusiano na Mlezi ………………………………
8. Kazi ya Baba/Mlezi (mkulima/mfanyakazi/mfanyabiashara) ………………
9. Kama ni mfanyakazi, kazi yake ni …………………………
10. Kama ni mkulima zao muhimu analolitegemea ni ………………
11. Kama ni mfanyabiashara, biashara yake ni ……………………
12. Jamaa katika familia:
    i. Idadi ya Kaka …
    ii. Idadi ya Dada …...
    iii. Wewe ni wangapi katika familia ….
    iv. Shule unayotoka ………..…...Wilaya ………………………
    v. Ukiwa shuleni utapanga au utakaa na Mzazi/Mlezi jina (kwa wale wa kutwa) ………………………………
    Mtaa ……………………………….
    Wilaya ……………………………………
    vii. Andika majina ya jamaa watatu ambao wako karibu watakaoweza kutoa msaada pindi wahitajiwapo shuleni
        a) Jina……………………………Anuani………………………
           Simu…………………………...
        b) Jina……………………………Anuani………………………
           Simu …………………………...
        c) Jina ………………………………. Anuani ……………………...
           Simu ……………………
    ii. Sahihi yako …………………………………

Futa lisilo husika

O/R TAMISEMI
SHULE YA SEKONDARI MLINGANO
FOMU YA KIAPO CHA URAIA

Kijana ………………………………………………………
Shule ya msingi……………………………………………
Namba ya mtihani ………………………………………
Mimi Mzazi / Mlezi wa mtoto …………………………….

Naapa kwa moyo wa dhati nikisema:

1. Mimi……………........................kazi………………ninaishi………………Wilaya… ……………………………………… Tanzania.
   Kwamba mimi ni Baba/Mama/Mlezi wa……………………... aliyezaliwa tarehe …………… katika kijiji / mji ……………….…. Na nilikuwa nikiishi katika kijiji hiki/mji huu wakati wa kuzaliwa kwa ………………………… na ninaikumbuka vyema siku hiyo.
2. Tarehe na mahali alipozaliwa havikuandikishwa kwa mujibu wa sheria katika muda wa miezi mitatu kwa kuwa haikuwa sheria ya lazima kwa jambo hili.

   Ameapishwa mbele yangu saa …………… tarehe ……………………… siku ya ………………. mwezi ………………mwaka…………………...
   Hakimu …………………………………………………………………

Official Stamp

FOMU YA UTHIBITISHO

……………………………………..
……………………………………..
……………………………………..

Mkuu wa shule
Shule ya sekondari Mlingano
S.L.P 281
MUHEZA

Barua hii ya tarehe ………………………. Nimeipata na ningependa kuwa hakikishia ninaikubali / siikubali nafasi hiyo niliyopewa kuingia kidato cha kwanza mwaka ……………………….

a) Nitaleta vifaa vyote muhimu vilivyotajwa katika fomu
b) Nitazitii na kuzinagtia sheria za shule kama itakavyoamriwa na walimu na wote wanaohusika kwa kufuata matakwa ya Shule na Serikali.

Kama anuani ilivyoandikwa hapo juu si anuani ya nyumbani kwetu utakapokwenda wakati wa likizo, basi andika hapa chini mahali utakapokuwa unakwenda wakati wa likizo kwa wazazi wako……………………………………

Wenu.

Jina la mwanafunzi (mwanao)………………………………………
Jina la Mzazi / mlezi …………………………………………………

# MEDICAL CERTIFICATE FORM

To be completed by the medical officer in respect of FORM ONE Entrant
Pupil's full name ………………………………………………………………

Age ☐ Sex ☐

Blood group court (Red and white)
……………………………………………………………………………………………………
Stool examination
……………………………………………………………………………………………………
Urine analysis
……………………………………………………………………………………………………
Syphilis
Test……………………………………………………………………………………………………
T.B Test
……………………………………………………………………………………………………
Eye Test
……………………………………………………………………………………………………
Ears Test
……………………………………………………………………………………………………
Chest
……………………………………………………………………………………………………
Spleen
……………………………………………………………………………………………………
Abdomen
……………………………………………………………………………………………………

ADDITION INFORMATION: e.g. Physical defects or impairment, infection chronic or family disease e.t.c
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
……………………………………………………………………………………………………
I certify that above is fit / unfit for admission into a day / boarding school
Signature ………………………………………………….
Designation ……………………………………………….
Station …………………………………………………….
Date ……………………………………………………….

OFFICIAL STAMP